# TARGETER WINGS

## JUNIOR SECONDARY SCHOOL ASSESSMENT

## GREDI YA SABA - 2024

Wings 002

**Muda: Saa 1 dakika 20**

# KISWAHILI

**Jina** ______________________________

**Shule** ______________________________

**Nambari ya Usajili:** ____________________ **Tarehe** ____________________

**Instructions:**

*(a) Andika jina lako, la shule, nambari ya usajili na tarehe kwenye vihasho uliopewa.*

*(b) Jibu maswali yote kwenye karatasi hili.*

| MTAHINI PEKEE | | | |
|---|---|---|---|
| **Swali** | **Upeo wa alama** | **Alama ya mwanafunzi** | **Kiwango cha utendaji** |
| 1-30 | Alama 50 | | |
| **Jumla** | **50** | | |



CamScanner

***Swali 1 hadi 4***

**UFAHAMU WA KUSOMA**



Hapo zamani za kale, mzee mmoja aliyekuwa na sherehe nyumbani kwake alienda kuazima sufuria kwa jirani. Aliahidi kumrejeshea jirani sufuria yake baada ya siku chache. Kutokana na ujirani mwema kati yao, jirani alikubali na kumpa sufuria bila vikwazo vyovyote.

Kwa kuwa ahadi ni deni, sherehe ilipokamilika alitimiza ahadi yake kwa kumrudishia jirani sufuria yake. Ajabu ni kuwa, mzee yule aliweka sufuria ndogo ndani ya ile kubwa wakati wa kuirejesha. Jirani alishangaa na kuamua kumrudishia mzee sufuria ndogo.

Mzee hakuipokea bali alimweleza kuwa sufuria ile kubwa ilipata mimba na kujifungua ndogo. Basi akamhakikishia kuwa ile sufuria ndogo ilikuwa yake. Jirani akafurahia sana na kumwambia awe akiazima sufuria mara nyingi atakavyo.

Mwezi mmoja ukapita, mzee akarejea kwa jirani kuomba sufuria. Alikuwa na sherehe ya harusi ya msichana wake. Jirani alimpa bila kusita kwa matarajio makubwa. Jirani akasubiri kwa siku kadha kurudishiwa sufuria na mtoto lakini wapi! Siku, majuma na miezi kadhaa baadaye bado sufuria haikuwa imerudishwa "Labda sufuria ilizaa mapacha." Alizidi kujiliwaza.

Hofu ikamzidi jirani na akaamua kwenda kwa mzee kumwuliza yaliyojiri. Alipofika kwa mzee alipigwa na butwaa mzee alipomwambia kuwa sufuria zote zilifariki wakati ile kubwa ilikuwa ikijifungua na tayari alikuwa ameizika pamoja na mtoto wake.

**1.** Kwa nini mzee aliazima jirani yake sufuria?

________________________________________

**2.** Jirani alikuwa na uhusiano mzuri na mzee. Andika kitendo kimoja alichofanya kuthibitisha kauli hii.

________________________________________

**3.** Unafikiri jirani angekosa kumpa mzee sufuria alipoenda kuazima mara ya pili ni jambo gani lingetokea?

________________________________________

**4.** Unajifunza nini kutokana na hadithi hii?

________________________________________

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali 5 hadi la 8.***



Usalama wa mwanafunzi shuleni ni muhimu sana. Wanafunzi wanapocheza shuleni wanapaswa kudumisha usalama wa wenzao ili mmoja asimsababishie mwenzake jeraha. Kurusha mawe ovyoovyo shuleni ni hatari. Vitisho kwa wanafunzi wageni vinapaswa kupigwa marufuku shuleni na hata njiani.

Udhalilishaji wa wanafunzi ni jambo hatari kwa mfano, mwanafunzi anapoulizwa swali na mtoto mwingine akacheka au akasema ni swali la kipumbavu, mwanafunzi huyo hawezi kuona vizuri. Mara nyingine mwanafunzi anapojaribu kujibu swali au kueleza jambo, wengine humcheka. Baadhi humcheka namna anavyotamka maneno, wengine kwa kutumia lugha isiyo sanifu na zumbukuku hucheka sababu wenzao wanacheka. Kitendo hiki kinaweza kumfanya mwanafunzi kutomakinika darasani na kuhofia kuuliza swali wakati mwingine. Usalama wake unahatarishwa.

Usalama unastahili kudumishwa shuleni kwa kuripoti visa vyovyote vya utovu wa nidhamu ili vishughulikiwe kwa wakati ufaao. Aidha inamjuza mwanafunzi ateue marafiki kwa makini ili asijiunge na kikundi cha wahalifu ambapo anaweza kupatikana kwenye makosa na akapigwa mtaani au kutumia dawa za kulevya zinazoweza kuhatarisha usalama wake.



CamScanner

5. Wanafunzi wanapocheza shuleni wanapaswa kudumisha usalama wa wenzao ili

______________________________________________

6. Ni mambo gani yanayoonyesha kuwa wanafunzi wanachangia usalama wa wenzao shuleni?
   A. Kucheka wenzao, kuripoti utovu wa nidhamu, kuteua marafiki wema.
   B. Kutorusha mawe, kutolisha wenzao, kutocheka.
   C. Kuripoti fujo shuleni, kulinda wenzao wasiumie na kutodhalilishana.
   D. Kuepuka uhalifu, kudhalilishana, uteuzi mzuri wa marafiki.
7. Uteuzi mzuri wa marafiki utazuia mambo gani? ______________________________
8. Kisawe cha neno **'dhalilisha'** ni
   A. fedhehesha B. vitinisha C. chukisha D. dharaulisha

**UFUPISHO**

***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 9 hadi 12.***

Usafi wa kibinafsi ni muhimu kwa kila mwanadamu, usafi wa kibinafsi unahusisha mambo mawili: Kwanza ni usafi wa mwili na la pili ni usafi wa mahali tunapoishi.

Ili mtu awe safi, inampasa aoge, achane nywele zake, akate kucha ndefu na apige mswaki. Mtu ambaye haogi wala kupiga mswaki hunuka na huwa chukizo kwa watu. Nguo anazovaa mtu zinapaswa kufuliwa na kupigwa pasi. Mtu akiwa msafi hatawaudhi watu anaoishi nao. Aidha atakuwa amejikinga dhidi ya magonjwa mengi.

Usafi utakuwa kamili nyumba unayoishi inapofagiliwa au kupigwa deki. Takataka hazifai kuwepo chumbani mwako. Ni bora uanike mablanketi na hata godoro na sharti yawe safi. Mazingira yote tunamoishi sharti tuhakikishe kuwa ni safi.

9. Andika kichwa kinachofaa kifungu hiki. ______________________________
10. Taja mambo mawili makuu yanayohusisha usafi wa kibinafsi.

    ______________________ ______________________
11. Andika ujumbe wa aya ya pili kwa sentensi moja. ______________________________
12. Neno **'hatawaudhi'** limetumika katika kifungu. Maana yake ni ______________________

**SARUFI**

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 13 hadi 17. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Mwanadamu anafanya kazi __13__ ajimudu maishani. Binadamu yeyote anataka kuishi maisha __14__. Ili kuafikia __15__ hilo sharti ujikaze kisabuni kwani __16__. Hakika, __17__ ya mwanadamu ni uwezo wake wa kujikidhia mahitaji ya kimsingi.

13. A. ndio B. hivyo C. ili D. ndiyo
14. A. njema B. jema C. chema D. mema
15. A. kitu B. lengo C. wajibu D. jukumu
16. A. mgaagaa na upwa hali wali mkavu. B. mchelea mwana kulia hulia mwenyewe.
    C. umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. D. mchuma janga hula na wa kwao.
17. A. dhamana B. dhamani C. thamini D. thamani

***Kuanzia swali la 18 hadi 27, jibu swali kulingana na maagizo.***

18. Kapu hili lina nomino za aina mbalimbali. Andika nomino ya kitenzi -jina iliyo kwenye kapu hili.






CamScanner

19. ***Jaza nafasi kwa kutumia viambishi vifaavyo:*** (alama 2)
Maji ya mvua ___________liyohifadhiwa mtungi _______ memwagika.

20. ***Andika ukanusho wa sentensi ifuatayo:***
Neema angalicheza mechi hiyo, timu yetu ingalishinda.

_______________________________________________

21. ***Jaza nafasi ya jedwali kwa kufuata mfano:***

| **Sentensi** | **Kinyume** |
| --- | --- |
| Talanta yake ilimletea **faida** | Talanta yake ilimletea hasara. |
| Waombolezaji wana **furaha** | _______________ |

22. ***Geuza sentensi iwe katika hali ya udogo:***
Chupa ya mtoto ilianguka _______________

23. ***Kamilisha sentensi:***
Hadhira ni kwa watazamaji kama vile kicha ni kwa _______________

24. ***Geuza sentensi ifuatayo iwe katika hali ya masharti -'ki'-***
Wakulima wangeandaa mashamba yao msimu huu wangepanda.

_______________________________________________

25. ***Bainisha matumizi ya kikomo katika sentensi ifuatayo:***
Bw. Onyango ni kocha hodari, ameongoza timu nyingi kushinda mecha zao.

_______________________________________________

26. ***Andika upya sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo:***
Charo alimnunulia Salome rinda zuri.
Andika kwa neno: Salome _______________

27. ***Unganisha sentensi zifuatazo kuwa sentensi moja sahihi:***
Katana anatazama runinga     Tatu anasoma kitabu cha hadithi.

_______________________________________________

**Fasihi (alama 20)**

28. ***Jibu maswali yafuatayo:***
a) Eleza maana ya maneno yafuatayo: (alama 3)
i) Fasihi (alama 1) _______________
ii) Fasihi simulizi (alama 1) _______________
iii) Fasihi andishi (alama 1) _______________

29. Andika tungo tano za fasihi simulizi. (alama 5)

_______________ _______________
_______________ _______________
_______________

30. a) Taja sifa tatu za fasihi andishi. (alama 3)

_______________ _______________
_______________

b) Andika sifa tatu za fasihi andishi. (alama 3)

_______________ _______________
_______________

c) Andika tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. (alama 3)

_______________ _______________

d) Novela ni nini? (alama 1)

e) Andika sifa mbili za novela. (alama 2)



CamScanner

Umepanga kuandaa sherehe ya kusherehekea siku ya kuzaliwa kwako. Sherehe yenyewe itafanyika mwezi wa Aprili. Unakusudia kumwalika rafiki yako. Andika barua ya kumwalika kuhudhuria sherehe hiyo.



CamScanner